

JAMHURI YA MUUNGANO TANZANIA
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
TAASISI YENYE VIWANGO VYA **ISO 9001:2015**



MATOKEO YA MNADA WA MASAFI KWA AJILI YA MAWASILIANO YA SIMU NA INTANETI

Kwa kuzingatia Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172 na Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura ya 306 ya Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambazo zinaipa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) nguvu ya kupanga, kugawa, kutoa, kuchukua, kusimamisha matumizi, kufuta au kwa namna yoyote ile kurekebisha mgawo wa masafa miongoni mwa watumiaji au wenye leseni za masafa ya mawasiliano; Mamlaka imefanya mnada wa masafa kwenye bendi za 700 MHz, 2300 MHz, 2600 MHz na 3500 MHz ambayo yanatumika kwa ajili ya mawasiliano ya simu na intaneti (International Mobile Telecommunication – IMT) kwa kuzingatia kanuni na miongozo ya Shirika la Mawasiliano Duniani (International Telecommunication Union - ITU).

Katika kutekeleza Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016, TCRA, pamoja na majukumu mengine, ina jukumu la kuhakikisha matumizi ya masafa yanaleta manufaa yafuatayo kwa Taifa: -

- a) Kuendeleza miundombinu ya mawasiliano ya kasi ili kuchochea maendeleo ya uchumi wa kidijiti katika sekta zote ikiwemo uchumi wa bluu.
- b) Uwezeshaji wa shughuli za kijamii na kiuchumi kwenye utoaji wa huduma kama vile elimu, afya, kilimo, biashara, huduma za kifedha n.k;
- c) Kupunguza gharama za utoaji huduma za mawasiliano kutokana na kubana matumizi kwa kuweka miundombinu michache zaidi kwa ajili ya kufikia maeneo mengi zaidi na hivyo kuwa na uwezekano wa kushusha bei kwa watumiaji;
- d) Kuendeleza ubora wa huduma za mawasiliano kwa watumiaji;
- e) Kueneza utoaji wa huduma za mawasiliano ya kasi kwa Watanzania wengi zaidi, hasa walio maeneo ya vijijini;
- f) Kushajihisha, kuendeleza na kuwezesha ubunifu wa huduma mpya za TEHAMA na matumizi yake; na
- g) Kuwa chanzo cha mapato kitaifa kwa kuzingatia kuwa masafa ni rasilimali adimu ya Taifa.

TCRA inatangaza kwa umma matokeo ya mnada huu uliofanyika tarehe 11 Oktoba 2022 kwa mafanikio makubwa. Jumla ya watoa huduma za mawasiliano watano (5) walishiriki kwenye mnada huo, na watoa huduma wanne (4) wameshinda masafa katika bendi tofauti kwa idadi ya vitalu kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini: -

Na.	Mtoa huduma	Bendi	Idadi ya vitalu	Jumla ya Mapato (Dola za Kimarekani)
1	Vodacom (T) PLC	700 MHz (FDD)	1	25,548,468.98
		2300 MHz (TDD)	2	34,378,597.94
		2600 MHz (TDD)	1	3,300,000.00
2	Airtel (T) PLC	3500 MHz (TDD)	2	21,100,001.02
		2600 MHz (FDD)	2	39,000,200.00
3	MIC (T) PLC (Tigo)	3500 MHz (TDD)	2	34,000,000.00
4	Viettel (T) PLC (Halotel)	2600 MHz (FDD)	1	30,169,000.00
Jumla ya mapato ya mnada (Dola za Kimarekani)				187,496,267.94

TCRA inawapongeza **Vodacom (T) PLC, Airtel (T) PLC, MIC (T) PLC, na Viettel (T) PLC** kwa kushinda na kupata masafa kwenye bendi za 700 MHz, 2300 MHz, 2600 MHz na 3500 MHz.

IMETOLEWA NA:

**Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania,
Na 20 Barabara ya Sam Nujoma,
SLP 474,
14414 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 241 2011-2
Nukushi: +255 22 2412009 Barua-pepe: dg@tcra.go.tz**